



MAFUNZO JUU YA UTAWALA WA HASIRA

MAHALI

UKUMBI WA KATA, KATA YA KILUNGULE
WILAYA YA TEMEKE DAR ES SALAAM

TAREHE

02/ NOVEMBER 2023

WASHIRIKI
VIONGOZI WA
KATA KILUNGULE

Hamisi Mwanaulanga
MTENDAJI KATA WEO (Ward Executive Officer)

Thereza J. Sinwa
AFISA MAENDELEO KATA CDO (Community Development Officer)

Noha G. Zongwe MEO - KWA MZUNGU

Charles C. Lukiko AO (Assitant Oficer)

Mwanate Khatib Akida MEO - KILUNGULE

Farida A. Mbaramwezi MEO - ZOMBOKO

Eneth E. Kajia EHO - ENVIRONMENTAL HEALTH OFICCER Kilungule

Mr. Huki MEO - MAJIMATITU B'

AGENDA

- Kufungua Mafunzo kwa Sala
Bi. JOYCE Mwampyate
- Utambulisho **MTENDAJI KATA**
- Mafunzo juu ya UTAWALA WA HASIRA
Mr. Projestus E. Rwegarulila
- MAJADIRIANO
- kufunga mafunzo

KUFUNGUA
MAFUNZO

Baada ya sala fupi iliyoongozwa na Bi. Joyce Mwampyate, Mtendaji kata ya Kilungule ndugu **Hamis Mwanaulanga** alikaribisha wajumbe na kutoa utambulisho wa taasisi ya PROFA FOUNDATION kwa viongozi wa kata. Kisha katibu mkuu wa PROFA alianza kueleza mahusiano ya mazingira na hasira, ya kwamba tunapopatwa na hasira, tunahitaji mazingira mazuri yenye utulivu ili KUSHUSHA HASIRA ZETU. "Mazingira ya mjini mengi ni chanzo cha hasira badala ya kuwa tiba ya hasira"

*Karibuni
Profa Foundation*

NAMNA YA KUFIKA
PROFA FOUNDATION

*"Watoto ni rafiki
wa mazingira"*



Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam

Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

Muwezesaji ndugu Projestus Rwegarulila alianza kwa kusema kwamba yeye hayuko hapa kuzuia watu wasikasirike bali yuko hapa kutoa elimu ya pindi tupatapo hasira tujisaidieje. Alitupitisha katika topic mbalimbali katika kujifunza namna ya kutawala hasira zikiwemo:

1. Hasira ni nini
2. Historia ya hasira
3. Takwimu za kidunia juu ya hasira
4. Hasira kwa Tanzania
5. Matumizi ya vilevi katika kupambana na hasira
6. Mpango wa kuzuia hasira
7. Tiba ya hasira



Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam

Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

WATOTO WA PROFA DAYCARE NAO WALISHIRIKI KWENYE ZOEZI LA KUPANDA NA KUTUNZA MAZINGIRA LILILOFANYIKA KATIKA SHULE YA MATERN LUMBANGA





Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es Salaam
Tell: +255 654 795 833 +255 762 044 791 Email: profafoundation@gmail.com

UFADHILI WA MASOMO

Profa Foundation ni shirika lisilo la kiserikali (NGO)
REG:00NGO/R/5092 linalofanya shughuli zake mtaa wa
Majimatitu B' katika kata ya Kilungule wilaya ya Temeke
mkoa wa Dar es salaam.

**SHIRIKA LINAPENDA KUWATANGAZIA
WANANCHI JUU YA UFADHILI WA MASOMO
YA AWALI (DAY CARE) NAFASI 10**

Masomo yataanza 06 MAY 2024 Wahi sasa

VIGEZO:

1. Miaka 2 - 5
2. Awe Yatima
3. Awe analewa na mzazi mmoja tu.

MAWASILIANO

0654 795 833, 0762 044 791

**Wajumbe walipewa nafasi ya kuuliza maswali na haya ni
baadhi ya maswali walio yauliza.**

- *Mjumbe alipongeza kwa namna semina ilivyoendeshwa na akasema ina manufaa na si kwa watu wazima tu, bali hata watoto wetu hasa vijana wapewe kipaumbele kwaajili ya kujifunza namna ya kutawala hasira.*
- *Mjumbe ameuliza kwamba iwapo utaratibu wa kwamba kama bibi na bwana wamekosana kitendo cha bwana kuondoka kwenda kulala hotelini kinaweza kuongeza madhara endapo ugomvi wenyewe ulikuwa unahusu nyumba ndogo?*
- *Mjumbe ameomba kama itawezekana kutoa elimu ya utawala wa hasira kwa kata zingine za wilaya ya Temeke.*
- *Mjumbe ameuliza utofauti kati ya utawala wa hasira na Afya ya akili.*

Muwezesaji alijibu maswali yote kwa ufasaha na wajumbe kuonekana kuelewa vizuri na kufurahia somo.

Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam

Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com



KUSAIDIA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM

KUANZA KUPOKEA WATOTO SHULE YA CHEKECHEA YA PROFA DAYCARE CENTRE



MAHALI

AGENDA

Kusaidia watoto wenye mahitaji maalumu, ni moja ya lengo la shirika letu la PROFA FOUNDATION. Na kwakuwa tunamiliki shule ya Chekechea ya PROFA DAYCARE CENTRE tuliona tuanze usajili wa watoto wenye mahitaji maalumu.

Ili kufanikisha hilo tulilazimika kutengeneza mabango na kuyatawanya mtaani kisha kuanza kupokea maombi. Kama bango linavyoonyesha tulihitaji kusaidia watoto wenye mzazi mmoja na pia YATIMA.

USHIRIKI WA SHULE YA PROFA DAYCARE KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'



USHIRIKI WA KITENGO CHA MALIASILI MANISPAA YA TEMEKE KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'



MAFUNZO JUU YA MAZINGIRA

MAHALI

UONGOZI NA WASHIRIKI

AGENDA

KUFUNGUA MAFUNZO

MAFUNZO JUU YA ULINZI WA MAZINGIRA

MAFUNZO JUU YA MAZINGIRA MAJIMATITU B'
KATA YA KILUNGULE WILAYA YA TEMEKE
15/ MARCH 2024

PROFA FOUNDATION
MAJI MATITU B (KATA YA KILUNGULE)
Temeke -Dar es salaam

Mkurugenzi mradi wa mafunzo **AMC Projestus Rwegarulila**
Mkurugenzi mradi wa Mazingira **Bi. Jossyeane Mwesigwa**
Bi. Nisalile January Mwaipasi Mkurugenzi mradi wa watoto
Bi. Mariam Elinzoo Mwl. PROFA DAYCARE CENTRE
Bi. Salama Rashid Mwl. PROFA DAYCARE CENTRE
Mr. Danny Mpogole Mwanachama Profa foundation
Bi. Jovina Deusidedith Mweka azina Profa foundation
Bi. Joyce Mwampyate Mwanachama Profa foundation
Mr. Anfrey Dioniz Mwanachama Profa foundation
Bi. Witness Jailos Tanganyika Mtunza office
Mr. Huki Mwakilishi serikali ya mtaa Majimatitu
Mr. Rivard Deusideth Mwanachama Profa foundation

- Kufungua Mafunzo kwa Sala
Bi. Nisalile J. Mwaipasi
- Utambulisho **Projestus Rwegarulila**
- Mafunzo juu ya MAZINGIRA
Bi. Jossyeane K. Mwesigwa
- MAJADIRIANO
- kufunga mafunzo

Bi. Nisalile J. Mwaipasi Alitufungulia kwa sala
Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam

Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833
Email: profafoundation@gmail.com

UTAMBULISHO

Mafunzo yalianza majira ya saa 10:00 Jioni baada ya sala. Katibu aliwakaribisha wajumbe wa mafunzo kwa kumtambulisha kiongozi kutoka serikali ya mtaa na kisha kuruhusu kila mmoja kujitambulisha. Baadaye katibu alieleza kwanini tumeamua kutoa mafunzo ya mazingira siku hiyo ya Ijumaa. Alisema tangu PROFA FOUNDATION ianzishwe tumekuwa na mafunzo kuhusu swala la utawala wa hasira, na siku ya mafunzo hayo, idara ya mazingira haikupata muda wa kutosha kwasababu swala la mazingira hatuwezi kulitenganisha na utawala wa hasira.

MAFUNZO JUU YA MAZINGIRA

Katibu mkuu alimkaribisha mkuu wa idara ya Mazingira kutoa elimu. Mtoa elimu aliweza kueleza tunaposema ulinzi wa mazingira tunamaanisha nini. Alianza kutukumbusha baadhi ya topic zihusuzo mazingira kuwa ni:

Kazi si kupanda miti tu, bali hata kuhifadhi ile ya asili iliyopo.

Pia kuhakikisha tunajali mazingira yaliyo tuzunguka.

Kuhakikisha tunaendeleza zile sehemu za wazi zilizotengwa na mipango miji.

Tuwe na list ya maeneo ya wazi kwaajili ya kutengeneza bustani ili watu wawe wanapata kwenda kutuliza akili huko.

Kutomwaga taka za sumu sehemu yenye matumizi ya watu wengi kama vile vyanzo vya maji.

MAJADILIANO KWA WOTE

Kabla katibu hajaongoza majadiriano baina ya wajumbe, Alionyesha mwaliko ulioambatanishwa na bango la kwamba kesho yake tunaombwa kushirikiana na mashirika mengine kwenda kusafisha KURASINI BEACH aliwaomba wajumbe washiriki kesho alfajiri na mapema.

MBOLEA YA KUPANDIA



MITI ILIYO LETWA NA PROFA FOUNDATION



Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam

Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

USHIRIKI WA SERIKALI YA MTA A KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'



USHIRIKI WA NEMC KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'



Bango la mwaliko kuonyesha ushiriki wetu katika kusafisha ufukwe wa bahari wa kurasini siku ya tarehe 16/03/2024

Kurasini Beach CleanUp

2024
16 MARCH @ Kurasini Beach
 07:00 am - 11:00 am.

PARTNERS

PROFA


For More Information Call: 0714870002, 0679839583, 0615632993 | Bring your Reusable water bottle and Comfortable footwear

Chasimba Street, Plot No.54, Majimaitu B' Mbagala - Dar es salaam
 Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

Baada ya maelezo ya katibu, wajumbe walianza kuuliza ni vifaa gani tuliitaji kubeba wakati wa kwenda kusafisha ufukwe wa Kurasini. Katibu aliwaeleza kuwa ni pamoja na viroba walau 20, Gloves box 2, leki pamoja na mifagio. Hata hivyo mwenyekiti ilibidi atafute vifaa hivyo kutoka madukani kabla ya kesho yake.

Mjumbe mwingine alipendekeza kwamba tuanze kuwa tunaenda kwenye mashule jirani kuanza kusafisha maeneo na upandaji wa miti.

Pia mjumbe aliuliza kama tunafahamu juu ya maeneo ya wazi yaliyotengwa na serikali. Alijibiwa kwamba tumeandika barua kwa mkurugenzi kuomba kujua maeneo ya wazi ili tuweze kuyatunza.


Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam
Teli: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

9/01/2024

MKURUGENZI
MANISPAA YA TEMEKE
P.O. BOX 46343
TEMEKE – DAR ES SALAAM

YAH: OMBI LA KUPEWA MAENEO YALIYO YA WAZI KATIKA WILAYA YETU ILI TUYAENDELEZE KWAAJILI YA WAKAZI WA TEMEKE KUPUMZIKIA

Ndugu,
Husika na kichwa cha habari, sisi PROFA FOUNDATION tunaomba kujua idadi na kupatiwa maeneo yaliyo ya wazi ili tuyabooneshe kwaajili ya wakazi wa Temeke kupumzikia wakati wa jua kali, kutuliza hasira pamoja na msongo wa mawazo.

Taasisi yetu inajihusisha na Mazingira, Utawala wa hasira pamoja na Haki za raia hasa watoto. Kwetu mazingira mazuri ni moja ya tiba ya hasira. Hivyo basi, sehemu za wazi zilizopangiliwa, kwa kupandwa miti, nyasi na maua mbali mbali, ni muhimu kwa wakazi wetu wa Temeke katika kutuliza Hasira.

Natanguliza shukrani zetu za dhati kwako kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza maeneo ya wazi kwa manufaa ya tiba ya hasira.

Ndimi katika ujenzi wa wilaya yetu,

Projestus Evarist Rwegarulila
EXECUTIVE SECRETARY
PROFA FOUNDATION

"IT CAN BE DONE PLAY YOUR PART"

Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam
Teli: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

SIKU YENYEWWE YA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B' TAREHE 28/5/2024

USHIRIKI WA WANAFUNZI KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'



USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA UPANDAJI MITI MAJIMATITU B'





SIKU YA UPANDAJI MITI SHULE YA MSINGI MAJIMATITU B' WILAYA TEMEKE DAR ES SALAAM

TAREHE

28 /MAY/ 2024

MATAYARISHO

**MFADHIRI SIKU
YA KUPANDA
MITI ENEO LA
MAJIMATITU B'**

On 29th, May 2024

*"Watoto ni rafiki
wa mazingira"*

MAHITAJI

- Maji ya kunywa kwa watu 500
- Soda kwa watu 500
- Vitafunwa (snacks) kwa watu 500
- T-shirts kwa watoto 150
- Gloves
- Gari ya matangazo
- Gari ya kubeba miche na mbolea

LENGO KUU

Kupanda miti kuzuia mmomonyoko wa udongo katika bonde la Majimatitu B' lililopo jirani na shule ya Matem Lumbanga Mbagala

*"Matern Lumbanga
yetu Kijani daima"* **May 28
2024** *"Watoto ni rafiki
wa mazingira"*

Logos of partner organizations: Mazingira Plus, Sana Mare, HUDEF, EQUITY, Muboko Charles Foundation, WISE, Good Deeds Day, YAGA KHAN FOUNDATION.

PROFA FOUNDATION, MAZINGIRA PLUS, SANA MARE, YOUTH WITH ENVIRONMENT, GOOD DEEDS, PRIME, TCCI, WISE, NEMC, MUTOKA CHARLES FOUNDATION, HUDEF, BRAC, TEMEKE MUNICIPAL, MBRC, MARINE PARKS, and many more.

BAADHI YA
MASHIRIKA
WASHIRIKI

Kufunga Mafunzo

MANENO YA MWAKILISHI WA SERIKALI YA MTA A KABLA YA KUFUNGA SEMINA:

"Twendeni tuyafanyie kazi yote tuliyo jifunza siku ya leo mkituhitaji pale mlikosahau tutafika kuwakumbusha, na kuwapa ushauri, mafunzo pamoja na misaada mingine iliyo ndani ya uwezo wetu.



Chasimba Street, Plot No.54, Majimatitu B' Mbagala - Dar es salaam
Tell: +255 654 795 833 +255 615 165 833 Email: profafoundation@gmail.com

SIKU YA UPANDAJI MITI SHULE YA MSINGI KISIWANI WILAYA YA KIGAMBONI

MAHALI

SHULE YA MSINGI KISIWANI WILAYA
YA KIGAMBONI - DAR ES SALAAM

TAREHE

14 /APRIL/ 2024

NASAHA

Maneno ya mkurugenzi wa PROFA FOUNDATION aliyoyatoa siku hiyo ya upandaji miti.

“Ndugu Watanzania, hizi mvua zina-zosababisha mafuriko pamoja na kuharibu miundo mbinu, joto kali kama tulilo lisikia kipindi cha January na February yote hayo, ni kwasababu ya Tabia ya nchi ambayo kwa sasa tunaona matokeo ya mwanadamu kutokuwa rafiki wa mazingira. Kizazi chetu kimeshiriki katika kuaribu mazingira. Watoto wetu wanaoshindwa kwenda mashuleni kwasababu ya mafuriko hawana hatia. Basi tutumie maji hayohayo, mvua kupanda miti walau kumi kila mtu kabla mvua hazijaisha. Na tuwafunze watoto kuwa rafiki wa mazingira”

BAADHI YA
MASHIRIKA
WASHIRIKI

PROFA FOUNDATION, MAZINGIRA PLUS,
SANA MARE, YOUTH WITH ENVIRONMENT,
GOOD DEEDS, HUDEFU, BRAC, TEMEKE
MUNICIPAL, MBRC, MARINE PARKS, and
many more.



Mkurugenzi wa PROFA FOUNDATION akiwaonyesha watoto wa shule ya msingi Kisiwani namna ya kupanda mti kisha kuupa jina la mtoto mhusika mti huo kusudi aendelee kuutunza

